


DW Akademie Film Development Fund



Ufadhili wa Uendelezaji wa Filamu | Mwongozo

Ufadhili

1. Ufadhili huu unatolewa kwa watengenezaji wa filamu (waandishi / waongozaji) ambao wanakidhi vigezo vifuatavyo:

- Waliowahi kuongoza angalau filamu moja ya kutunga au makala au filamu fupi, ambayo imesambazwa nchini au kimataifa
- Awe raia wa nchi ambako wito wa maombi unafanyika,
- Anayeishi na kufanya kazi katika nchi husika.

Watayarishaji (Maprodyusa) hawastahiki kuomba.

2. Muundo wa filamu utakaokubalika kuombewa (Fomati) ni filamu za hadithi za kutunga au za makala na hata mahuluti (ya mchanganyiko kama docudrama)
(zisipungue urefu wa dakika 60)

3. Ufadhili ni kwa awamu ya maendeleo ya utengenezaji wa filamu kwa jumla. Awamu ya maendeleo ya hatua za mwanzo za filamu, lakini inaweza kuzidi, shughuli zifuatazo:

- Utayarishaji wa Mswada
- Utafiti
- Kutafiti maeneo na kutaka kujua uhusika kwa kina
- Kunadi mawazo
- Ufadhili kifedha
- Mwendelezo wa mikakati ya uuzaji na usambazaji

4. Watengeneza-filamu watakaochaguliwa watapokea hadi €10,000 kwa awamu ya maendeleo ya filamu yao.

5. Ufadhili hautatolewa ikiwa shughuli ambazo zinaombewa ufadhili- kwa jinsi zilivyoelzwa katika mpangokazi wa mwombaji - tayari zimepokea ufadhili mahali pengine.

6. Miradi inayofadhiliwa lazima izingatie maadili ya Umoja wa Mataifa ya "Azimio la Haki za Binadamu" (UDHR). Miradi inayokiuka UDHR kwa, kwa mfano, kushabikia vita, kukazia unyanyasaji kimwili, kisaikolojia au kijinsia, au kukera hisia za maudhui ya kijamii au dini, haitaungwa mkono.

DW Akademie Film Development Fund



Kipimo cha utayari kwa mafunzo ya DW Akademie

DW Akademie itafadhili mpangokazi wa ushauri, pamoja kutoa mafunzo ya aina mbalimbali. Watengenezaji wa filamu waliochaguliwa ni lazima wawe tayari kushiriki angalau 80% ya siku za ushauri na mafunzo yatakatolewa.

Mchakato wa maombi na nyaraka zinazohitajika kwa usaili

1. Waombaji lazima wawasilishe maombi yao kwa ukamilifu na katika kipindi kilichowekwa.

Tarehe ya kufunga maombi ni Oktoba 25, 2021 na nyaraka zitakazowasilishwa ni:

- Mwongozo wa filamu
- Fomu ya maombi (mtandaoni)
- Ratiba ya kazi
- CV

Waombaji wa miradi ilioteuliwa kushindanishwa wanaweza kuulizwa kuwasilisha yafuatayo:

- Toleo la hivi karibuni la mwongozo wa filamu au skripti
- Bajeti

DW Akademie itawasiliana na waombaji ambao miradi yao imeteuliwa. Hili litafanyika takriban wiki tatu baada ya kufunga maombi.

Maombi yasiyokamilika hayatazingatiwa.

2. Hairuhusiwi kuwasilisha maombi kwa mradi zaidi ya mmoja.

3. Hakuna sheria itakayohusu ufadhili

Mkataba na utoaji fedha

1. DW Akademie itatoa mkataba kwa kila mtengenezaji wa filamu aliyechaguliwa.

2. Fedha za ufadhili zitatolewa kwa awamu.

3. Maelezo ya kina kuhusu ufadhili wa mradi yataianishwa katika mkataba utakaohitimishwa baada ya uteuzi kufanyika.

Hakimiliki zote za mawazo yaliyowasilishwa zitabaki kwa wamiliki asili wa haki zile.

Isipokuwa kama imeainishwa vinginevyo katika mkataba.